# Lugha Ishara katika Dhifa za Jikoni (*Kitchen Party*) Nchini Tanzania

Doroth F. Mosha


## Ikisiri

Makala hii inahusu lugha ishara katika dhifa za jikoni nchini Tanzania. Makala imejikita zaidi katika kuzibaini na kuzifasiri lugha ishara na namna zinavyojidhihirisha kitamathali hasa zile zinazoundwa kisitiari na kitashibiha. Wafundaji katika dhifa za jikoni huwa na mbinu bunifu za kuunda ishara hizo na imebainika kuwa vifaa vya upambaji na baadhi ya zawadi zitolewazo kwa mwari huashiria maana fulani kimuktadha. Dhifa za jikoni ni uwanda ambao unahitaji kuchimbwa kwa kina kitaaluma na kiutafiti kutokana na umuhimu wake katika maisha ya jamii hususani maisha ya ndoa. Dhifa za jikoni zimeibuka kutokana na tofauti zilizopo za maisha ya ndoa kati ya mume na mke na hata jamii na jamii. Benokraitis (2008) ana maoni kuwa taratibu za ndoa zinatofautiana baina ya jamii moja na nyingine kwa sababu wanajamii wa kila jamii hujijengea utamaduni unaoeleza kaida ambazo zinafafanua dhana ya ndoa. Data za makala hii zilikusanywa kwa kuhudhuria dhifa mbalimbali za jikoni jijini Dar es Salaam kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji wa ushiriki. Baadhi ya data zimechukuliwa katika tasnifu ya mtafiti. Uchambuzi wa data umeongozwa na Nadharia ya Mwitikio wa Wasomaji/Wasikilizaji.


## 1.0 Utangulizi

Dhifa ni sherehe na dhana inayoweza kuelezwa kulingana na miktadha tofauti katika ngazi ya kitaifa na kijamii. Katika muktadha wa kumfunda mwari, sherehe zinazofanyika huweza kutafsirika kwa dhana ya '*dhifa za jikoni*' kwa sababu zawadi nyingi apewazo ni vyombo vya kutumika jikoni. Dhifa za jikoni kwa Kiingereza '*Kitchen Party*' na kwa jina lililozoeleka nchini Tanzania ni sherehe wafanyiwazo wari ambazo huambatana na mafunzo mahususi yanayohusu maisha ya ndoa. Katika sherehe hizi, wari hupewa zawadi zinazohusiana na ama chumbani au kutumika jikoni. Ni katika hili pia ambapo familia zenye kujiweza kiuchumi humwandalia mwari mahitaji yote ya nyumba kama vile samani, nguo, vyombo vya jikoni na kadhalika. Dhifa za jikoni hufanyika katika jamii mbalimbali nchini Tanzania. Tofauti ya sherehe hizi ni ndogo sana kati ya jamii moja na jamii nyingine. Hii ni kutokana na utamaduni wa jamii husika alimolelewa mwari na ni kwa sababu kila jamii ina utamaduni unaojibainisha na jamii nyingine. Lakini pia kila jamii ina desturi za kiutamaduni zinazojumuishwa katika sherehe hizo na kuzifanya ziwe tofauti, kwa mfano matumizi ya nyimbo za kitamaduni na lugha ya jamii husika.

Utafiti wa makala hii ulifanyika mwaka 2012. Mtafiti alihudhuria sherehe zipatazo kumi. Utafiti ulilenga kuzifasiri lugha ishara katika dhifa za jikoni ambazo zimeonekana kuhusiana kwa kiasi kikubwa katika jamii mbalimbali nchini Tanzania. Mjadala umelenga hasa kuchunguza lugha ishara zinazoelezwa kitamathali, yaani zinazojibainisha katika tashibiha na sitiari. Hii ni moja kati ya mitindo mahususi ya lugha inayotumika katika kuwasilisha mafunzo ya ndoa na ambayo haiwezi kufafanuliwa vema bila ya kuzingatia utamaduni, miktadha na

matumizi yake. Halliday (1964) anasema kuwa tamko la lugha haliwezi kueleweka ipasavyo ikiwa litafasiriwa pekee pasipo kuhusishwa na masuala mengine ya muktadha, hali ya watu waliohusika, mahusiano kati yao, mada inayozungumziwa, mazingira na masuala mengine ya mawasiliano.

Makala inaongozwa na Nadharia ya Mwitikio wa Wasomaji ambayo msomaji huwa na mawazo juu ya matini anayoipitia, yaani msomaji anatazamiwa kuipokea kazi ya fasihi kwa kuzingatia mielekeo yake binafsi (Abrams, 1999; Wafula, 2007). Wanamwitiko wanaamini kwamba msomaji hugundua mambo kadhaa kwa kujiuliza maswali yatakayomwonyesha majibu ya mafumbo aliyofumbiwa. Katika nadharia hii sifa bainifu za kazi yenyewe yaani msimulizi, wahusika, mtindo, muundo na maana hufinyangwa na kupangwa upya kwa mujibu wa tajiriba ya msomaji. Maana ya matini huumbwa na kuzalika upya na hivyo hakuna maana moja au fasiri zinazofanana kwa wasomaji wa kazi moja. Nadharia hii imetumika kuchambua maana za lugha ishara zinazojidhihirisha kisitiari na kitashibiha katika dhifa za jikoni nchini Tanzania. Mtafiti amefasiri maana hizo kulingana na tajiriba yake na muktadha wa mazungumzo yaliyowasilishwa katika dhifa hizo za jikoni.

Makala hii ina sehemu kuu tano. Sehamu ya kwanza ni utangulizi ambao unazungumzia kwa ufupi kuhusu dhifa za jikoni na muhtasari wa nadharia inayoongoza makala hii. Sehemu ya pili inahusu utendaji wa dhifa za jikoni kwa maana ya utaratibu mzima wa kufanyika kwake. Sehemu ya tatu imeangazia mafunzo yatolewayo katika dhifa za jikoni. Sehemu ya nne imejikita kwenye kiini cha mada kinachohusu lugha ishara zinazojibainisha kisitiari na kitashibihi. Sehemu ya tano na ya mwisho imetoa hitimisho kuhusu matokeo ya utafiti, na umuhimu wa lugha ishara.

## 2.0 Utendaji katika Dhifa za Jikoni

Dhifa za jikoni huadhimishwa katika kumbi mbalimbali za starehe na katika mazingira ya vijijini na mijini nchini Tanzania. Wahusika wa sherehe hizi hukodi ukumbi na kuulipia kiasi fulani cha fedha walizokubaliana na mmiliki wa ukumbi. Ukumbi huo huweza kupambwa kwa maua na vitambaa vyenye rangi zinazofanana na rangi za nguo anazovaa mwari, msaidizi wake na wageni waalikwa. Hii ni namna ya kupendezesha ukumbi. Aidha, mapambo ya kiutamaduni hujumuishwa kwa kuzingatia utamaduni wa mwari ijapokuwa mapambo hayo hufanana kwa kiasi kikubwa baina ya jamii moja na jamii nyingine. Hii ni pamoja na matumizi ya nyungo, shanga, visonjo, mafiga ya mawe, vyungu, mikeka na kadhalika. Vilevile vyakula vya asili hutumika kama mapambo, lakini vikiwa vimebeba ishara muhimu kimuktadha. Mara nyingi sherehe hizi hufanyika nyakati za jioni au usiku kati ya saa kumi jioni na saa tano usiku hususan siku za mwisho wa juma. Siku hizi ni nzuri kwa kuwa ni za mapumziko kwa walioajiriwa na hivyo hufanya mahudhurio ya wageni waalikwa kuwa makubwa kutokana na usemi wa wengi kuwa ‘shughuli ni watu’.

Maandalizi ya dhifa za jikoni huwa na utaratibu ufuatao; siku moja kabla ya siku ya sherehe, mwari hupewa mafunzo mazito yenye usiri mkubwa na wahusika wa mafunzo hayo ni shangazi, bibi na watu wengine wa nasaba. Baadhi ya jamii hutafuta mfundaji na kumpatia kiasi fulani cha fedha kwa ajili ya kumfunda mwari wao. Mafunzo wanayompatia mwari hayatofautiani sana kimaudhui na mafunzo yanayotolewa na mtoa mada na wageni waalikwa wakiwa ukumbini. Tofauti ya msingi iliyobainika ni matumizi ya usiri kwa kuwa mwari hufunzwa masuala mazito yasiyotumia mafumbo (ya wazi) ambayo hayapaswi kuwekwa hadharani ambayo wakati mwingine huambatana na vitendo. Katika mazingira ya ukumbini mafunzo hayo hurahisishwa na kuwasilishwa kijuujuu kwa kufumbata maana lengwa. Kwa namna fulani kuna mwingiliano wa baadhi ya mambo katika sherehe hizi na sherehe za unyago kwa wasichana ambazo hufanywa na jamii nyingi nchini. Hata hivyo, ni vema ifahamike kwamba dhifa za jikoni na sherehe za unyago ni vitu viwili tofauti. Baadhi ya wanajamii hudhani kuwa sherehe za unyago zimebadilika na kuzalika kwa sherehe za kisasa ambazo ni dhifa za jikoni. Sherehe za unyago ziko palepale na bado zinaendelea kufanyika katika jamii mbalimbali kwa mfano, Wazaramo, Wamatumbi, Wazigua, Wamasai, Wamakonde na kadhalika. Kinachoonekana ni mwingiliano wa sherehe hizi mbili ambapo dhifa za jikoni katika kufanyika kwake zimekopa baadhi ya mambo kutoka katika sherehe za unyago ambazo ni kongwe.

Siku ya sherehe mwari hupelekwa saluni na kupambwa na wakati unapowadia mwari huanza safari kuelekea ukumbini. Mwari haruhusiwi kuingia ndani ya ukumbi kabla ya wageni waalikwa wote kuwasili ukumbini. Mshereheshaji huanza kwa kuwakaribisha kina mama waalikwa ukumbini, huku wakicheza na kusindikizwa kwa nyimbo mbalimbali (za dini, asili, bongofleva nk). Mwari na msaidizi wake hukaribishwa baada ya wageni waalikwa kuingia ukumbini, huku nao wakisindikizwa kwa muziki wowote ama wimbo wa kiutamaduni waliochaguliwa, vifijo na vigelegele kutoka kwa akinamama waalikwa.

Mshereheshaji huanza kwa kutoa utambulisho kwa mwari na msaidizi wake, kisha kumkabidhi mwari kipazasauti ili atambulishe wazazi, ndugu jamaa na marafiki. Baada ya utambulisho, wageni waalikwa huburudika kwa vinywaji vilivyoandaliwa. Mwari hualikwa kukata keki iliyotengenezwa kwa unga wa ngano na kuwalisha wazazi na watu maalum walioandaliwa. Baada ya tukio hilo, mshereheshaji humkaribisha mtoa mada (mfundaji) aliyealikwa rasmi kutoa mafunzo kwa mwari. Wakati wa uwasilishaji wa mafunzo hayo dhana ya utendaji na muktadha wa uwasilishaji (Mulokozi, 1996) hujidhihirisha kwa uwazi kama mbinu muhimu katika kazi za fasihi simulizi. Mfundaji hutumia ishara za mwili katika kuzungumza na kuufanya ujumbe kuwa hai kutokana na matumizi ya vitendo, na hata kuishirikisha hadhira yake. Tazama mfano huu:

Mtoa mada: *Kina mama mwari wetu amependeza hajapendeza?*
Kina mama: *Amependeza.*

Mtoa mada: *Wenye wivu……..*
Kina mama: *Wajinyongeeee!* (Data za uwandani, 2013)

Hapa mtoa mada anaishirikisha hadhira yake kwa lengo la kuvuta usikivu wa akina mama kwa yale atakayoyazungumza. Vilevile mbinu hii ni kama kitangulizi cha kujiandaa kabla ya kuwasilisha ujumbe husika kwa mwari na kwa hadhira.

Halikadhalika, mama, bibi, shangazi na dada wa mwari hupewa nafasi ya kumfunda mwari kulingana na malezi waliyompa na kwa kuzingatia utamaduni husika. Baada ya kila mmoja kuzungumza, wageni waalikwa (akinamama) hukaribishwa ili kusema kile kilichosahaulika na mtoa mada na ndugu wa mwari. Katika sherehe mojawapo iliyohudhuriwa na mtafiti, mshereheshaji alisikika akisema '*ni wakati sasa wa kuziba mapengo*', akimaanisha kuwa wakati umewadia wa wageni waalikwa (kina mama) kuzungumza kile ambacho kimesahaulika. Mafunzo katika dhifa za jikoni huwasilishwa kwa lugha ya Kiswahili na hadhira yake kubwa ni kina mama na baadhi ya vijana wa kike wachache kuanzia umri wa miaka kumi na minane. Vijana hawa huruhusiwa kwa kigezo cha kuwa ndugu na rafiki wa karibu wa mwari na kuwa nao wamefikia umri wa kuweza kuolewa.

Hatua inayofuata baada ya mafunzo ni mwari, msaidizi wake pamoja na wageni waalikwa kula chakula. Muziki wa taratibu huendelea kutumbuiza wakati wa chakula. Baada ya chakula, wageni waalikwa hupewa nafasi ya kucheza muziki, zikiwamo nyimbo za taarabu na nyinginezo. Zawadi hutolewa kwa mwari baada ya muziki na baadhi ya zawadi huambatana na maelezo yenye ishara fulani. Zawadi nyingi zinazotolewa ni vyombo vya jikoni na baadhi ni nguo, mikeka na kadhalika. Baada ya zawadi, muziki huendelea kutumbuiza huku akina mama na mwari wakiendelea kucheza na kuburudika kwa vinywaji. Mwisho mshereheshaji huhitimisha sherehe kwa kumuaga mwari na kumtakia maisha mema ya ndoa. Wageni waalikwa nao huondoka ukumbini kurudi makwao.

## 3.0 Mafunzo katika Dhifa za Jikoni

Kila jamii ina taratibu zake za malezi kwa watoto. Watoto huelekezwa kulingana na jinsi. Rothman (1987) ana maoni kwamba wanaume na wanawake huelekezwa tofauti tangu wanapozaliwa. Watoto wa kiume huelekezwa kazi wazifanyazo baba zao ilhali watoto wa kike hufunzwa kazi wanazofanya mama zao. Malezi haya husababisha wakue na kujitwika majukumu kulingana na jinsi zao. Suala hili pia hujitokeza hata katika fasihi ya watoto hususan katika nyimbo za watoto wakati wa michezo yao na vitabu vya hadithi (taz. Omari, 2008; Lyimo, 2014).

Katika dhifa za jikoni, mafunzo yanayotolewa ni pamoja na kumwandaa, kumwelekeza, kumsajilisha na kumwingiza mwari katika masuala ya unyumba. Mafunzo katika jamii mbalimbali za Watanzania hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya masimulizi ya mdomo yanayojumuisha mbinu anuwai mfano tamathali za semi, methali, misemo, nahau na vipengele vingine vya fasihi simulizi. Mwari hufunzwa mambo mbalimbali kama vile upishi, usafi, elimu ya

uzazi, mahusiano mazuri na majirani na ndugu wa mwanamume, na namna ya kumhudumia na kumtunza mume. Hoja hii pia inajitokeza kwa Lott (1994) anayesema kuwa mwanawake hufunzwa namna anavyotakiwa kukamilika kwa kuwa mke na mama, yaani kuzaa na kulea watoto. Naye Zastrow (1997) anasema kuwa wanawake wanapaswa kukaa nyumbani kumtunza mume na watoto na wala si kujishughulisha na ulimwengu wa siasa. Mtazamo wa Zastrow (khj) unapingwa na wanawake wa ulimwengu wa sasa ambao wanapinga vikali pingu hizi za kiutamaduni.

Aidha, mafunzo hujumuisha pia namna ya mwanamke kuwa kivutio kwa mume. Njia ya kufanikisha hili ni pamoja na kuvaa mavazi ambayo ni ya kisasa, kujipaka manukato, kuwa na furaha kila wakati mume awapo nyumbani, kutabasamu, kumheshimu na kukubali yale mume anayoelekeza kwa mke (taz. pia *Utenzi wa Mwanakupona*).

Suala la dini yamkini halisahauliki wakati wa kumfunda mwari. Wanawari huelezwa kuwa wamshirikishe Mwenyezi Mungu katika kuombea ndoa zao ili ziweze kuwa na baraka na pia zidumu. Ni kutokana na hali halisi ya namna ndoa zilivyo na matatizo mengi katika jamii. Haya pia yamesemwa na Mitman (1980) anayeeleza kwamba ni Mungu ambaye amewaunganisha mwanamume na mwanamke katika ndoa. Mungu anashirikishwa kulinda ndoa na huwapenda wale wanaooana. Pia, huishi katika imani yao na kuwabariki katika mahusiano yao. Mafunzo katika sherehe hizi yameelezwa kwa ufupi ili kupata picha halisi ya yale yanayofunzwa na kuyahusisha na ishara zilizoainishwa na kufanyiwa uchambuzi katika makala hii.

## 4.0 Lugha Ishara

Lugha huwa haitoi ujumbe wa maneno pekee, bali hueleza hisia, nia na thamani ili kuthibitisha uhusiano na desturi za jamii husika. 'Katika hali yake ya kuzungumzwa na kuandikwa, ama kwa ishara au mazungumzo lugha ndicho chombo cha kumbukumbu, tamaduni, maarifa na ujuzi.'[1] Ishara ni ile hali ya kitu fulani kumaanisha kitu kingine. Kwa hiyo lugha ishara ni ile ambayo inatumia jina la kitu kimoja kumaanisha kitu kingine (Alembi, 2000; Samwel, 2012). Kulingana na wataalam hawa ni kwamba, ishara hutolewa kwa namna mbili; mosi, ishara kama kitu / kifaa au picha kwa mfano zawadi alizokabidhiwa mwari ziliwasilishwa kiishara kwa kutumia kauli kama vile '*Nakukabidhi kinu na mchi ukavitumie vizuri katika kutwanga*.' Hapa kinu na mchi ni vifaa vinavyoashiria maana fulani. Kwa mujibu wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji/Msikilizaji / hadhira hutumia tajiriba zao kufasiri maana iliyofumbatwa katika vifaa hivyo. Mtafiti kama miongoni mwa hadhira wenye tajiriba yake anatupa fasiri ya kinu na mchi kuashiria sehemu za siri za mwanamke na mwanamume na kutwanga kuashiria kufanya tendo la ndoa. Pili, ishara katika muktadha wa lugha. Huu ni uzungumzaji unaotumia maneno yenye

[1] www.unesco.org/culture/ich iliyosomwa 22/10/2012.

ishara fulani. Ninaweza kusema 'mapenzi ni dhahabu' nikiashiria kuwa mapenzi ya dhati ni adimu kama ilivyo adimu kuyapata madini ya dhahabu. Ishara hutumiwa kuelezea kitu fulani katika kazi ya kifasihi ambacho huwakilisha kingine. Kuwakilisha huku kunaweza kutokana na uhusiano uliopo kati ya vitu hivyo viwili au uwezo wake wa kuibua fikira fulani katika akili ya msomaji (Wamitila, 2003). Ishara na mazungumzo huwa na mwingiliano wa aina yake. Ishara hutegemea mazungumzo katika kuwasilisha ujumbe kwa walengwa. Mazungumzo nayo kama utanzu wa fasihi simulizi huwa na ishara ndani yake kwa kuwa ni kazi ya kisanaa. Dhifa za jikoni hutumia mazungumzo ya kisanaa kama asemavyo Mulokozi (1996) kuwa ili mazungumzo yawe ya kifasihi, lazima yawe na usanii wa aina fulani, yaumithilishe uhalisi badala ya kuunakili. Mazungumzo huwa na vipengele vya mawasiliano kwa ishara vinavyojulikana kama ‘*viziada-lugha*’ ambavyo huhusisha ubora wa sauti, vifaa, vionjo vya mwili na sifa ya msisitizo. Dhifa za jikoni zimesheheni ishara ambazo nyingi zimetokana na vifaa vya upambaji na zawadi apewazo mwari. Wafundaji hutumia mazungumzo kisanii kutoa ufafanuzi wa vifaa hivyo vyenye athari kubwa kwa mwari na wasikilizaji. Lengo ni kuufanya ujumbe unate ipasavyo katika ubongo wa mwari na hadhira kwa ujumla.

Tanzania ni nchi yenye makabila mbalimbali yenye utamaduni wa kumpa mwari zawadi wakati wa kumfunda. Zawadi hizo huwa ni vyombo vya jikoni na vitu vingine kama vile nguo, mashuka, vitambaa vya mezani na kadhalika. Pamoja na kuwa sherehe hizi huitwa dhifa za jikoni, baadhi ya zawadi zinazotolewa kama zilivyotajwa hapo awali si zile tu zinazohusu muktadha wa jikoni bali pia huhusu zawadi nyingine muhimu kwa matumizi ya wanandoa na familia yao. Zawadi hizo hupelekwa ukumbini sehemu ambayo imepangwa kumpatia mwari mafunzo. Baadhi ya zawadi huwa na ishara fulani katika muktadha wa maisha ya ndoa. Aidha, sehemu inayopambwa kwa ajili ya mwari kukaa huwekwa baadhi ya vifaa vya kitamaduni vya jamii husika ambavyo huwa na ishara fulani. Dundes (1965, 1980, 2002) ana hoja kuwa matini zinazowasilishwa katika sherehe mbalimbali hubeba matini ishara za kitamaduni. Kwa mantiki hiyo, makala hii imeweka bayana baadhi ya ishara zinazojitokeza kisitiari na kitashibiha wakati wa kumfunda mwari.

### 4.1 Sitiari kama Nyenzo ya Ishara

Sitiari ni tamathali ya usemi ielezayo sifa ya kitu fulani kwa kusema kuwa ni kingine. Ni mbinu ya ulinganishi isiyotumia viungo ‘kama’, ‘mfano wa’, ‘mithili ya’, na kadhalika (Wamitila, 2003, 2008). Sitiari huhusisha dhana mbili tofauti na hujengeka katika kuhamisha maana na kujenga picha au taswira fulani akilini mwa msomaji au msikilizaji. Aidha, sitiari huweza kubeba ishara ndani mwake ambayo kwayo huleta maana fiche. Hivyo basi, jamii ya watu wanaoishi wakiwa na uhusiano wa karibu na mazingira halisi, ishara huibuka kutoka katika mazingira yao (Swantz, 1974). Sitiari na ishara ni dhana zinazohusiana kwa kuwa zote zinajumuisha uziada wa maana. Kauli hii imeungwa mkono na Paul (1976) kuwa

sitiari ndiyo hasa kibainishi kiletacho dhana ya ishara ambayo ina mvuto katika lugha na hufanya kazi ya uziada wa maana. Sitiari na ishara husababisha mawazo anuwai, yaani fasiri za mawazo zisizokuwa na idadi maalum kama ambavyo wanamwitiko wa msomaji wanavyotoa hoja kuwa maana ya matini huumbwa na kuzalika upya na hivyo hakuna maana moja au fasiri zinazofanana kwa wasomaji wa kazi moja. Sitiari huleta maana za ndani za ishara katika lugha na hutabiri mtindo ambao ndani mwake ishara huhifadhiwa. Jamii ya Watanzania huzingatia baadhi ya ishara za kisitiari zenye uhusiano na mazingira mwari alikolelewa. Hapa zimeorodheshwa baadhi tu ya ishara za kisitiari za msingi katika sherehe zilizohudhuriwa na kuzitolea ufafanuzi:

### 4.1.1 Mlango

Dhana ya mlango ilitokana na kauli iliyotolewa na mmoja wa wafundaji kwa kueleza yafuatayo:

> *Sasa wewe umekuwa mlango wa mume wako tu. Mume atautumia mlango huu kuingia na kutoka…* (Data za uwandani, 2011).

Katika hali na maana ya kawaida mlango hutumika kuingilia na kutokea. Mlango unapofungwa si rahisi mtu kuingia ndani. Katika dhifa hizi za jikoni mwari kuoneshwa mlango ni kiashiria cha kuyakubali maisha ya ndoa na kamwe mke hapaswi kusema hapana pindi mume anapomhitaji katika tendo la ndoa. Kulingana na Lott (1994) tabia za namna hii huelekezwa kuwavutia wanamume. Mwari huaswa kuwa anapaswa kumhudumia mumewe tu katika tendo la ndoa na asigeuke kuwa mlango kwa kila mwanamume anayemtaka kimapenzi.

### 4.1.2 Mazao na Vyakula Mbalimbali

Mazao kama vile mahindi, ndizi, mpunga, maharage, muhogo, nyanya, pilipili, matango, nazi, matunda, mboga za majani na mengineyo mengi hulimwa katika jamii mbalimbali nchini Tanzania. Wapambaji katika sherehe za kumfunda mwari hutumia mazao hayo na vyakula mbalimbali kupamba sehemu anayokaa mwari wakati wa kumfunda. Sherehe inapomalizika mama mzazi / mlezi wa mwari au mtu yeyote muhimu wa nasaba yake kama vile shangazi hukabidhiwa mazao hayo. Hiyo ni ishara kuwa, mwanamke mwenye uwezo wa kuwa na watoto ni sawa na ardhi yenye rutuba ambayo imeweza kumea vyakula hivyo. Tuangalie kauli ifuatayo:

*Tunakukabidhi vyakula hivi vikakufae na uvifae pia…*(Data za uwandani, 2011)

Kimsingi kauli hiyo, kwa mfano, inaposemwa na mama, ni ishara iliyowalenga wajukuu ambao mwanae atakwenda kuwazaa. Waafrika wana falsafa inayoamini suala la uzazi baada ya mwanamke kuolewa hivyo katika utamaduni wa jamii za Kitanzania mwanamke anapoolewa anatarajiwa kupata watoto. Hili linatiliwa mkazo sana. Wajukuu wanaotarajiwa kwa mwari watakuwa msaada kwa bibi kwa kumsaidia shughuli mbalimbali na bibi atapata fursa ya kuwapa malezi kama

wajukuu zake. Si ajabu kumkuta bibi ndiye mlezi mkuu wa mjukuu kuliko mama mzazi wa mtoto katika baadhi ya familia. Huu ni utamaduni uliozoeleka miongoni mwa baadhi ya jamii za Waswahili/Watanzania.

Aidha, tunda aina ya papai lilikatwa na ndani mwake mna nyama nyekundu, mbegu nyeusi na utomvu mweupe. Kila kimoja kati ya hivi kina ishara kulingana na muktadha husika wa sherehe hiyo. Nyama nyekundu ni ishara kamili ya uke. Mbegu nyeusi ni kiashiria cha mbegu za kiume ambazo tayari ziko ndani ya uke ilhali utomvu mweupe ni uteute mweupe unaopatikana katika uke wa mwanamke. Kimsingi nyama nyekundu, mbegu nyeusi na utomvu mweupe ni dhana zinazounda ishara kamilifu ya tendo la ndoa kati ya mwanamume na mwanamke. Katika moja ya sherehe niliyohudhuria mwari alikabidhiwa papai lililokatwa sawia na kupewa maelezo haya:

> *Tunakuomba upokee papai hili ulikague ndani mwake kwa umakini. Mwanetu, huko ndiko kukua…*(Data za uwandani, 2013)

Kwa kutafakari kauli hiyo hapo juu, mfundaji alikuwa na dhana kuwa mwari amekuwa mtu mzima kwa kuwa amebalehe na viungo vyake vya uzazi vimekomaa kiasi cha kuwa na uwezo na fursa ya kukutana kimwili na mwanamume na kuzaa watoto. Hata hivyo, suala la mwanamume kutokuwa na uwezo wa kuzaa halikupewa nafasi kana kwamba limesahaulika katika sherehe hizi. Ni vema mwari afahamishwe kuwa uwezo wa kutunga mimba na kuzaa watoto unaweza pia usiwapo kutokana na sababu za kibiolojia ama matatizo ya kiafya kwa mwanamume na mwanamke.

### 4.1.3 Dhana ya Upendo, Faraja na Athari zake

Dhana ya upendo ina nafasi kubwa katika mafunzo yanayotolewa kwa mwari nchini Tanzania. Dhana hii ni pana katika maisha ya wanadamu yenye kukamilishwa na mambo makuu manne; kuishi kwa pamoja, kushirikiana, kusaidiana na kuthaminiana. Mambo haya huwafanya wanadamu kuishi kwa furaha na faraja. Kinachowaunganisha wanandoa katika mahusiano yao ni upendo unaozaa faraja katika mioyo yao. Upendo unapokosekana baina ya mume na mke ndoa huingia katika misukosuko ya namna nyingi. Baadhi ya sitiari za kiishara zenye maudhui ya upendo katika sherehe zilizohudhuriwa ni; *mume / mke ni mwanga wa maisha yako* (mume / mke ndiye anayeifanya ndoa iwe na upendo, furaha na faraja) ambayo ni sawa kimaudhui na sitiari *yeye ni tufaha la macho yako* (mume / mke wako kipenzi) na *mapenzi ni dhahabu* (mapenzi yana thamani na ni nadra kumpata mwenzi mwenye upendo wa dhati kama ilivyo dhahabu na upatikanaji wake).

Aidha, upendo unapokosekana katika maisha ya ndoa (wanandoa kutothaminiana na kutoshirikiana) madhara yake huwa ni ugomvi ndani ya nyumba na wakati mwingine kusababisha utengano kwa wanandoa. Katika sitiari

*'mapenzi wakati mwingine ni mwiba'* na *'maisha ni chombo kipitacho juu ya mawimbi ya bahari'* zinathibitisha hayo na kumhadharisha mwari kuwa makini. Uvumilivu, busara na subira ni silaha kwa wanandoa endapo hali hiyo itajitokeza kwa kuwa ukamilifu wa maisha na ndoa hupimika katika mafanikio na matatizo.

### 4.1.4 Zawadi Anuwai

Mafunzo yanayotolewa kwa mwari hutokana pia na zawadi anazokabidhiwa. Mwari huzawadiwa vyombo vya jikoni ambavyo vitamfaa katika maisha mapya ya ndoa. Baadhi ya vyombo hivyo vinaashiria dhana mbalimbali katika maisha ya ndoa. Hapa vimechukuliwa vyombo vichache na vya msingi na kutolewa ufafanuzi kwa mfano mwiko, sufuria, kinu na mchi, ungo, sahani, chujio, nazi na kibao cha kukunia nazi (mbuzi). Wawasilishaji hutoa maelezo ya kila chombo kwa kuufumbata ujumbe husika kwa mwari na hadhira kwa ujumla. Jambo la msingi ni kuwa vifaa vilivyotajwa vinaashiria dhana ya tendo la ndoa na umbo la viungo vinavyohusika katika tendo hilo la ndoa. Kwa mfano, mwiko, mchi, na kibao cha kukunia nazi ni viashiria vya uume ilhali sufuria, kinu, nazi, chujio, ungo, sahani ni viashiria vya uke. Tuangalie kauli hii iliyotolewa na mmoja wa wafundaji:

> *Nakukabidhi sufuria na mwiko wake ukavitumie kumpikia mumeo chakula. Kwa mfano unaposonga ugali, hakikisha umeugeuza ipasavyo ili ugali ulainike vizuri. Zungusha mwiko wako uguse kila kona ya sufuria. Baada ya kuepua ugali wako, safisha mwiko wako na sufuria kwa utaratibu…*
> (Data za uwandani, 2013)

Kwa kuisoma kauli hiyo hapo juu mtafiti ameufinyanga ujumbe kwa tajiriba yake na kufasiri upya kuwa mwasilishaji alitoa kauli hiyo akiwa na maana ama taswira nzima ya dhana na mchakato mzima wa tendo la ndoa. Na katika sentensi ya mwisho, anamaanisha kuwa baada ya tendo la ndoa mke hana budi kumweka mume katika hali ya usafi na pia kujiweka safi yeye mwenyewe. Nihitimishe hapa kwa kusema kuwa sitiari nyingi zinazojitokeza katika dhifa za jikoni zilizohudhuriwa na mtafiti baadhi hujirudia kwa namna tofauti. Kadhalika nijikite katika tashibihi na kuzitalii baadhi ya ishara zilizobainika.

### 4.2 Tashibihi kama Nyenzo ya Ishara

Dhana ya tashibihi imefasiliwa na Wamitila (2003) kuwa ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia waziwazi. Tashibihi hutambulishwa na matumizi ya viungo 'kama', 'mfano wa', 'mithili ya' na kadhalika. Kutokana na sherehe zilizohudhuriwa na mtafiti, ishara za kitashibihi zilizobainika ni chache zikilinganishwa na zile za kisitiari. Tashibihi nyingi zilizojitokeza katika dhifa za jikoni zimefafanuliwa kwa lugha nyepesi na zenye maana ya wazi. Tajiriba ya

mtafiti imetumika kufinyanga upya ishara za kitashibihi na kutoa maana mbalimbali. Hapa zimefafanuliwa ishara chache tu za kitashibihi.

### 4.2.1 Karata Nyeusi na Nyekundu (cheusi chekundu)

*Maisha ya ndoa ni mithili ya cheusi chekundu…*(Data za uwandani, 2011)

Kauli hiyo hapo juu ilitolewa na mmoja wa kina mama waalikwa. Katika tashibihi hii, cheusi chekundu ni mchezo wa kamari wenye karata mbili za rangi nyeusi na nyekundu. Karata hizo hufunikwa ili kumpa nafasi mchezaji kutambua kati ya rangi hizo mbili. Mchezaji akigeuza karata nyekundu hupewa fedha mara mbili ya zile alizotoa na akigeuza karata nyeusi hupoteza fedha alizotoa. Huu ni mchezo wa kubahatisha (bahati nasibu). Katika muktadha wa kumfunda mwari, nyenzo hii ni ishara yenye maana kuwa maisha ya ndoa yanahitaji busara, umakini na uvumilivu. Ni maisha ambayo yakifanyiwa mzaha husababisha matatizo chungu nzima kama vile ugomvi, utengano, kifo na mengine mengi. Vilevile, cheusi chekundu ni ishara kuwa maisha ya ndoa ni kama mchezo wa bahati nasibu, yaani mke au mume anaweza kubahatika kwa kumpata mwenzi mwenye tabia nzuri au mbaya. Kwa vile pia ameshaingia mkataba wa kuishi maisha ya ndoa, hana budi kuwa mvumilivu kwa mwenzi wake kwa kuukubali udhaifu wake na kutafuta mbinu za kiustarabu za kukabiliana na hali hiyo.

### 4.2.2 Njiwa

*Maisha yenu ya ndoa yawe kama njiwa huyu alivyoing'ang'ania sumaku…*(Data za uwandani, 2011)

Hii ni tashibihi yenye ishara ya njiwa. Mfundaji alimtumia njiwa bandia aliyeng'ang'ania sumaku. Njiwa huyo ni ishara ya mume na sumaku ni mke ambaye ndiye atakayeimarisha na kuipalilia ndoa ama kuibomoa. Dhana hii pia, imezungumzwa katika kitabu kitakatifu cha biblia kuwa mwanamke mpumbavu huibomoa ndoa yake kwa mikono yake mwenyewe. Mke anapokuwa na heshima kwa mume na kumhudumia vilivyo, ni vigumu kwa mume kuichoka ndoa na kupoteza uaminifu kwa mwenzi wake. Mke ndiye anayepaswa kumlea mume ikiwa ni pamoja na kumtunza aonekane nadhifu machoni pa watu. Zastrow (1997) amesema kuwa wanawake wanapaswa kukaa nyumbani kumtunza mume na watoto na wala si kujishughulisha na ulimwengu wa siasa. Mawazo yake yanapingana na wanawake wa nyakati za sasa (wanaharakati). Wanaharakati wana mtazamo kuwa mwanamke ana haki ya kujishughulisha kama afanyavyo mwanamume kwa minajili ya kuleta maendeleo ya familia, jamii na taifa lakini akielewa majukumu yake kama mke na mama wa familia.

### 4.2.3 Chungu na Mwiko

*Unapotumia chungu na mwiko kupika usikae kama mtoto ajifunzaye kukaa. Utashindwa kupika vizuri na chakula hakitalika…*(Data za uwandani, 2013)

Ishara iliyokusudiwa hapa ni kwamba mwari anapaswa kuwa mbunifu wakati wa tendo la ndoa. Anapokosa ubunifu huo, hawatalifurahia tendo hilo na athari yake ni ukosefu wa uaminifu katika ndoa. Mikao ya namna tofauti wakati wa kushiriki tendo la ndoa huleta raha ya aina yake na ya kipekee kati ya mume na mke. Kwa kutumia lugha ishara hizi mwari anapewa mafunzo kuhusu nafasi yake katika maisha ya ndoa na katika kumridhisha mume.

### 4.2.4 Ndala na Kiberiti

Utafiti wetu ulibaini kuwa zawadi ya ndala na kiberiti zilitolewa kwa mwari zikiambatana na kauli hii: *Maisha ya ndoa ni sawa na ndala hizi na kiberiti hiki* (Data za uwandani, 2013).

Kimsingi, vifaa hivi hudharaulika sana lakini vinapokosekana umuhimu wake ndipo unapoonekana na kuthaminiwa. Ndala huvaliwa sana katika mazingira ya nyumbani ikiwa ni pamoja na kuendea msalani. Ifikapo nyakati za usiku ndala huachwa nje na thamani yake hupotea kwa wakati huo. Mwari aliaswa kuwa maisha ya ndoa yanahitaji uvumilivu mwingi mithili ya ndala kwa kuwa wakati mwingine mke huweza kudharaulika na mume na hata ndugu wa mume. Mke anapokuwa mbali na nyumbani umuhimu wake hudhihirika kwa wakati huo sawa na ndala zinapokosekana mtumiaji hawezi kupekua wala kuingia msalani. Mke ana nafasi ya kipekee katika ndoa yake. Halikadhalika, umuhimu wa kiberiti unaonekana tu wakati wa kuwasha moto au taa. Kimaudhui, kiberiti kikiwa kinawaka kinafananishwa na mke mwenye kuongea sana. Moto wa kiberiti huwaka kwa pupa na kuzima baada ya muda mfupi sana. Papara hizo hizo za kiberiti anakanywa mwari kuwa mdomo usio na busara hubomoa ndoa haraka sana.

## 5.0 Hitimisho

Katika makala hii tumeweza kubainisha lugha ishara zilizozingatiwa wakati wa kumfunda mwari katika jamii za Watanzania. Ishara hizo zimefasiriwa kwa namna zilivyoundwa kisitiari na kitashibihi. Uchunguzi umedhihirisha kuwa baadhi ya vifaa vya upambaji na zawadi apewazo mwari ni zaidi ya matumizi ya kawaida kutokana na ishara zilizomo katika muktadha wa maisha ya ndoa. Aidha, maudhui yaliyobebwa na ishara hizo yanalenga zaidi kuimarisha mahusiano kati ya mume na mke hasa katika tendo la ndoa. Maudhui mengine yaliyozungumziwa kupitia ishara hizi ni pamoja na namna ya kuishi na watu (heshima na adabu), uvumilivu, upendo na usafi. Kwa ujumla maudhui makuu ya maisha ya ndoa hubebwa na kuwasilishwa kwa njia ya ishara. Lugha ishara hizo hueleweka haraka sana kama zimechotwa kutoka katika mazingira na maisha ambayo wasikilizaji wameyazoea na wameyaishi. Dundes (2002) ana maoni kuwa wataalam wanaoshughulikia elimu (ya) jadi wana imani kwamba, ili kuelewa vizuri maelezo lazima kuchunguza muktadha hasa mazingira ambamo tukio linapatikana ama kutumika, mienendo,

imani na namna tukio linavyoelezwa. Hivyo basi, ishara hufasirika vizuri iwapo jamii lugha, utamaduni na mazingira yake yatazingatiwa.

Aidha, lugha ishara huleta mvutano baina ya usemi unaoeleweka waziwazi na ule ulio na maana fiche; yaani hutupa miundo ya ndani na ya kina ya uzungumzi. Lugha ishara hubeba ujumbe mzito kwa mwari na hadhira shiriki. Huwafanya waupate vizuri ujumbe uliokusudiwa na kuelewa maudhui kikamilifu, kwa kina na kwa njia fupi. Dhifa za jikoni ni uwanda ambao unahitaji tafiti zaidi za kitaaluma kutokana na majukumu yake mazito katika jamii zetu. Hata hivyo, kuna dosari chache katika sherehe hizi. Miongoni mwa dosari hizo ni pamoja na; dhifa za jikoni kuadhimishwa kwa muda mfupi, kutozingatia dhana ya usiri, kutozingatia hadhira yenye vigezo na kutokuwa na mwongozo maalum wa kutolea mafunzo (mtaala) kwa kuwa sherehe hizi haziko katika mfumo rasmi wa elimu. Kuna madai kuwa baadhi ya dhifa za jikoni hugubikwa na lugha chafu lakini kwa muktadha wa kazi za fasihi ni moja kati ya mbinu za kisanaa na ni jambo linalokubalika. Inafaa dosari hizi kufanyiwa kazi ili kuboresha sherehe hizi na kuzifanya ziwe na thamani kubwa katika jamii mbalimbali nchini Tanzania.

## Marejeleo

Abrams, M.H. (1999). *A Glossary of Literary Terms*. Boston: Eart McPeek.

Alembi, E.B (2000). *Understanding Poetry*. Nairobi: Acacia Publisher.

Benokraitis, N.V (2008). *Marriages and Families: Changes, Choice and Constraints.* New York: Pearson Education Inc.

Beidelman, T.O. (1986). *Moral Imagination in Kaguru Modes of Thought*. Bloomington: Indiana University Press.

Dundes, A. (1965). *The Study of Folklore.* Upper Saddle River: NJ Prentice Hall.

_____ (1980). *Who are the folk? In Interpreting Folklore*. Bloomington: Indiana UniversityPress.

_____ (2002). *Bloody Mary in the Mirror: Essays in Psychoanalytic Folklorists.* University Press of Mississippi.

Halliday, M.A.K. na wenzake (1964). *The Linguistic Science and Language Teaching*. London: Longman.

Lott, B. (1994). *Women Lives: Themes and Variations in Gender Learning*. Pacific Grove: C A Brooks.

Lyimo E.B. (2014). Usaguzi wa Kijinsia katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto na Mtazamo wa Wadau Nchini Tanzania. Shahada ya Uzamivu. Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mitman, J.L.C. (1980). *Primarital Counseling*: A Manual For Clergy and Counselors. Massachusetts: The Seabury Press.

Mosha, D. F (2011) Matumizi ya Lugha Katika Dhifa za Jikoni za Wazaramo. Shahada ya Umahiri. Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Omari, S. (2008). "Fasihi Simulizi na Jinsia: Mifano kutoka Nyimbo za Watoto Tanzania" katika *Kiswahili Juz. 71*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, uk 98-107.

Paul, R. (1976). Interpretation Theory: Discourse and the Surplus of Meaning. Texas: Texas Christian University Press.

Rothman, J. (1987). *Community Theory and Research in Encyclopaedia of Social Work*: Vol. 1: Silver Spring.

Samwel, M. (2012). *Hadithi Fupi: Nadharia na Mifano*. Dodoma: Kasenyenda.

Wafula, R. M. na K. Njogu (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

_____(2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Limited.

Zastrow, C. (1997). *Understanding Human Behaviour and the Social Environment.* Englewood Cliffs: NJ Prentice-Hall.

http://www.unesco.org/culture/ich. Iliyosomwa 22/10/2012

http://www.uiowa.edu~africart. Iliyosomwa 3/2/2013